# VIPENGELE VYA MUUJIZA WA QUR_ANI

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU
VIPENGELE VYA MUUJIZA WA QUR-ANI (2). A

Katika somo lililopita tulielezea na kukumbushana kuwa muujiza wa Qur-ani umegawika katika vipengele vitatu, vipengele hivyo ni muujiza wa mabainisho, muujiza wa kisheria, na muujiza wa kielimu, kipengele cha mwanzo ambacho ni muujiza wa mabainisho tulikielezea katika makala .iliyopita, na vipengele viwili vilivyobakia tutavielezea katika makala hii

:MIUJIZA YA KIELIMU ILIYOMO NDANI YA QUR-ANI .2

Makusudio yaliyokusudiwa katika muujiza wa kielimu ni ishara za kielimu zilizoashiriwa katika baadhi ya aya za Qur-ani, mabainisho hayo ya kielimu hayakuwa hadafu (madhumuni) asili katika ubainishwaji wake, kwa sababu Qur-ani ni kitabu cha uongofu, na hadafu au dhumuni asili ya kuteremshwa kitabu hicho ni kumfunza mwanaadamu njia za kuishi ili afikie katika saada ya Mwenyeezi Mungu na sio kubainisha masuala ya kielimu, kwa hiyo kama katika Aya za Qur-ani tutakabiliana na ishara za kielimu ni kwa sababu maelezo hayo yaliyomo ndani ya Qur-ani yametokana na elimu pamoja na hikima za Mwenyeezi Mungu. Kwa mfano katika -:Suratul-Furqan Aya ya 6 tunasoma

قُلْ اَنزَلَهُ الَّذِى يَعْلَمُ السِّرَّ فِى السَّمَاوَاتِ وَالاَرْضِ إِنَّهُ كَانَ غَفُوراً رَّحِيماً[1]

Sema: “Ameyateremsha haya yule ajuaye siri za mbinguni na ardhini; bila shaka Yeye ni mwingi ”.(wa msamaha(na) Mwingi wa rehema. (Lau kama si hivyo mngeona

Katika Qur-ani kumeashiriwa ishara nyingi za kielimu, baadhi ya ishara hizo zimeonekana kwa kupita muda, na pengine baadhi ya ishara nyengine nyingi za kielimu zinaweza kudhihirika kwa kupita muda mrefu, - wanaelimu – katika zama hizi – wamefanya jitihada sana katika masuala hayo, ijapokuwa kuna baadhi yao walikosea, ama vile vile wengi wao wamefanikiwa katika kuyathibitisha masuala kama hayo, mifano mengine ya ishara hizo za kielimu imeashiriwa katika kitabu cha Tamhiydiy, juzuu ya 6, na katika Kitabu cha Elimu ya Qur-ani, katika sehemu ya miujiza ya Qur-ani. Katika sehemu hii ili kufupisha maelezo tutaiainisha mifano miwili tu.

A. KUPATA TABU KUVUTA PUMZI KUTOKANA NA UZITO WANAOUHISI VIFUANI MWAO

-:Allah (s.w) katika suratul-Al-An-aam Aya ya 125 anasema

فَمَن يُرِدِ اللّهُ اَن يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلإِسْلاَمِ وَمَن يُرِدْ اَن يُضِلَّهُ يَجْعَلْ صَدْرَهُ ضَيِّقاً حَرَجاً كَاَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِى السَّمَاء كَذٰلِكَ يَجْعَلُ اللّهُ الرِّجْسَ عَلٰي الَّذِينَ لاَ يُؤْمِنُونَ[2]

Basi yule ambaye Mwenyeezi Mungu anataka kumwongoza, hufungulia kifua chake Uislamu; na yule ambaye Mwenyeezi Mungu anataka kumhukumu kupotea, hufanya kifua chake kizito kinaona tabu kubwa (kufuata huo uislamu); kama kwamba anapanda mbinguni (kusikokuwa na .pumzi). Namna hivi Mwenyeezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wale wasioamini

Aya hiyo inaelezea kuhusu tabu ya maisha watakayoipata wale watu waliopotea, watu hao wametolewa mfano na kufananizwa kuwa wanafanya jitihada kupanda juu (mbinguni), na kwa sababu ya tabu wanayoipata hushindwa kuvuta pumzi, na kujihisi kuwa vifua vyao ni vizito. Wafasiri wa zama zilizopita wamehitilafiana nadhari kuhusiana na Aya hiyo, baadhi ya watu ;hao wamesema kuwa

Makusudio ya Aya hiyo inamzungumzia mtu ambaye anafanya jitihada katika jambo ambalo haliwezekani katu kufanyika, mtu huyo anataka kuruka mbinguni kwa kutumia mbawa mfano wa ndege anavyoruka angani, ama kutokana na kwamba ni jambo lisilowezekana, hughadhibika na kukasirika, na kutokana na ghadhabu alizonazo hufikia hali ya kupata tabu na kushindwa -:kuvuta pumzi, na watu wengine wamesema

Mfananizo uliotolewa katika Aya hiyo, ni mfano wa miti michanga inayotaka kukuwa katika msitu ulio na miti mikubwa mikubwa, ama kutokana na kuwa katika msitu huo kuna miti ya .iliyosongamana na kushikamana pamoja, miti hiyo michanga haipati nafasi ya kukuwa vizuri

Maudhui hayo yaliyotolewa kutokana na Aya hiyo hayaleti ufahamu wowote utakaofafanua kwa ,uwazi kusudio la Aya hiyo

Ama kuna mtizamo mwengine wa elimu ya kileo unafahamisha zaidi maana ya Aya hii na kutowa ufafanuzi wenye muelekeo zaidi, kwa kutumia mtizamo wa kielimu unaohusiana na elimu ya kigeographia na elimu ya science kwa ujumla, kwani katika mtizamo wa kisayansi imeelezewa wazi kabisa kwamba mwanaadamu hawezi kunasibiana na hali ya hewa iliyoko angani, kwani kila anapoiwacha ardhi kwa masafa marefu zaidi ndipo hewa ya oxygen inazidi .(kutengana naye, na ni hali hiyo hiyo ukielekea chini ya ardhi (baharini

يَصَّعَّدُ فِى Makosa waliyoyafanya wafasiri wa zama zilizopita ni kuyafafanua maelezo ya Aya hii kuwa (فِى) na wameifahamu herufi ,(عين) na (صاد) kutokana na shida iliyopo katika – السَّمَاء inaleta maana ya - kwa ajili ya kupanda mbinguni - katika hali ambayo kama ikichukuliwa kilugha ,(يَصَّعَّدُ) na neno ,(فِى) badala ya herufi ,(الى) maana hiyo ni lazima ingelitumika herufi .(yaani (kupanda juu ,(صعود) lisingelikuwa na maana ya

tasaudu) lina maana ) ( (تصعد) (tafaulu) : ,(ثفعل) katika mlango wa – (يَصَّعَّد) Bali kutumika neno ya (kuwa katika tabu), na kutokana na kupata tabu huko humsababishia mtu kupata tabu katika .( ,(تصعد نفسه) kuvuta pumzi, na, katika istilaha za kilugha neno

tasaada nafsuhu) lina maana ya kuvuta pumzi kwa tabu, na kifua huhisi maumivu makali, na) lina maana ya kupata tabu, au lina maana ya jambo ambalo ni gumu ,(صعد) na (صعود) neno .sana

-:Katika Suratul-Jinni Aya ya 17 Allah (s.w) anasema

لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ وَمَن يُعْرِضْ عَن ذِكْرِ رَبِّهِ يَسْلُكْهُ عَذَاباً صَعَدا[3]

Ili tuwajaribu; (tuwafanyie mtihani) kwa hayo, na anayepuuza kumkumbuka Mola wake .atamsukuma katika adhabu ngumu

-:Na katika Suratul-Mudathir Aya ya 17 anasema

سَأُرْهِقُهُ صَعُوداً[4]

.Basi nitamtesa kwa mateso makuu

litakuwa na maana hii ifuatayo: yaani mfano ,يَصَّعَّدُ فِى السَّمَاء كَأَنَّمَا Kutokana na maana hiyo basi wa mtu aliyepanda juu sana, na kutokana na tabu hiyo ngumu atakayoipata atapata tabu katika .kuvuta pumzi

Kwa hakika yule mtu ambaye atapotea (atapotoka) katika njia ya Mwenyeezi Mungu atakuwa ni mfano wa mtu atakayepata tabu sana kwa kutaka kupanda juu (mbinguni), na katika hali hiyo .basi atapata tabu katika kuvuta pumzi

Kwa kuzingatia ufafanuzi wa Aya hiyo itafahamika kuwa maana hiyo tuliyoifafanuwa ni sahihi zaidi kulinganisha na zile nadharia zilizotolewa na baadhi ya watu. Kwa hiyo pindi itakapokuwa mtu atakosa njia ya kujihifadhia wakati anapopanda juu atakutwa na matatizo hayo ya kuvuta

pumzi, na kwa ishara ya masuala hayo katika zama zilizopita ilijulikana ni moja wapo katika .miujiza ya elimu ya Qur-ani

Suratul-Furqan Aya ya 6 [1]

suratul-Al-An-aam Aya ya 125 [2]

Suratul-Jinni Aya ya 17 [3]

Suratul-Mudathir Aya ya 17 [4]

MWISHO